



## EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

### OMBI LA KUONYESHA NIA: KUTOA HUDUMA YA USHAURI WA KITAALAMU KWA MRADI WA EACOP

TotalEnergies East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi, inaalka taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya Ushauri wa Kitaalamu kwa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili ili kusafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoani nane (8).

#### MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:

KAMPUNI inahitaji idadi ya washauri wataalam kusaidia Mradi ili kutekelezwa kwa kufuata viwango vya ufadhili vya kimataifa. Washauri wanahitajika katika nyanja zifuatazo;

- Utwaaji wa Ardhi na uhamishwaji usio wa hiari ikijumuisha upangaji na utekelezaji wa mpango wa uhamishaji; KUMBUKUMBU0010007270.
- Urejeshaji wa ustawi wa maisha ya watu kwa miradi mikubwa; KUMBUKUMBU 0010007264.
- Usimamizi wa Utendaji wa Jamii kwa miradi mikubwa ya miundombinu wakati wa ujenzi ikijumuisha utaalamu wa jinsia; KUMBUKUMBU0010007266.
- Mahitaji ya Viwango vya Kimataifa vya Ufadhili wa Mazingira na Afya ya Binadamu, Usalama na Ulinzi (EHSS) kwa miradi ya viwanda; KUMBUKUMBU 0010007267.
- Biashara na Haki za Kibinadamu ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi endelevu wa haki za binadamu kwa miradi mikubwa; KUMBUKUMBU0010007265.
- Ushauri wa Mahusiano ya Viwanda; KUMBUKUMBU 0010007269.
- Makundi ya Kikabila yanayoishi pembezoni wenye uzoefu wa kufanikisha makubaliano ya utoaji kibali cha utekelezaji baada ya utoaji taarifa (FPIC); KUMBUKUMBU 0010007268.

#### Kila mshauri anapaswa kuwa na:

- Angalau uzoefu wa miaka 20 katika eneo lao la utaalamu.
- Uzoefu wa katika utaalamu wa miradi mikubwa inayolingana katika muktadha wa ustawi wa Maisha unaohusiana na ardhi.
- Uzoefu wa kitaaluma katika nchi kadhaa tofauti ikiwa ni pamoja na Afrika Mashariki na Kusini.
- Awe ametoa huduma za ushauri kwa miradi iliyofadhiliwa na benki za maendeleo, benki za biashara na wakala wa mikopo ya nje ikijumuisha taasisi za fedha za ikweta. Experience of undertaking and managing.
- Uzoefu wa kufanya na kusimamia michakato na ukaguzi wa mkopeshaji wa mazingira na kijamii (utwaaji wa ardhi, utendaji wa kijamii, na ustawi wa maisha).
- Uzoefu wa kufanya kazi na mashirika ya kiserikali ili kufikia viwango vya kimataifa vya ufadhili juu ya utwaaji wa ardhi na urejeshaji wa ustawi wa maisha).
- Uzoefu wa kitaalamu wa majukumu ya ushauri wa kimkakati kwa Miradi mikubwa ya mafuta na gesi katika Afrika Mashariki utakuwa wa manufaa.
- Uwezo wa kusafiri kati ya Tanzania na Uganda mara kwa mara.

#### VIGZO MUHIMU:

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita. Kama unahusika.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye mradi huu na ujuzi na uzoefu wa kazi katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za programme.
- Kuzingatia Kanuni za fursa za wazawa za 2017 na ufafanuzi wa Kampuni za wazawa.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoordheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajiwa hapo juu kupitia barua pepe kwa

**[eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com](mailto:eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com)** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla saa **9:00** alasiri za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **6 Desemba 2021**. Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni kumbukumbu namba husika.

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.